# LBE KOMPUTA NA INTANETI- KIPINDI CHA 2

**Mwandishi : Richard Lough**

**Muhariri : Thomas Mösch / Katrin Ogunsade**

**Tafsiri: Eric Ponda**

**Wahusika :Mvula**na wa Makamu), Beatrice (Msichana wa Makamu), Komputa (sauti), Mtaalam (Sauti ya Mwanaume kutoka Studio)
**:** Timothy (Muuzaji wa Komputa kuukuu)
**Sauti:** Msimulizi kutoka Studio.

**Music – [Full up for 0:10 then fade under Intro]**

**Intro:**

Hujambo na karibu kwa mfululizo wa vipindi vyetu vya "Learning By Ear" kuhusu Komputa na Intaneti . Katika kipindi cha leo tutakupa vidokezo tu kuhusu mambo unayopasa kujua au kuuliza unapotnunua Komputa hasa ikiwa ni kuukuu. Pia utasikia kutoka kwa mtaalam wetu wa Intaneti kutoka sutdioni. Lakini kwanza John anakwenda moja kwa moja hadi kwa muuzaji wa Komputa kuukuu jijini Nairobi nchini Kenya

**Package 2.1**

**SFX_Katika karakana.**

**SFX_Mlango unafunguliwa [0:14]**

**Clip: 2.1_Timothy:** Habari yako, nikusaidieje***?***

**1. John:** Naitwa John. natafuta Komputa ya kuu kuu ninunue, ni gani inaweza kunifaa kwa kazi zangu za shule. Yaani Komputa ambayo pia naweza kuitumia kucheza michezo ya Komputa, kuhifadhi na kucheza Muziki na Video..

**Clip: 2.1**_Timothy : Sawa hapa niko na komputa ya ***Laptop*** aina ya ***Dell*** . Hii ni nzuri sana na inaweza kukusaidia ingawa imetumika. Vipimo ni vya juu sana . Na iwapo unatafuta Komputa ya vipimo hivi, basi hii ni nzuri sana. Vipimo vyake ni ***Ghz 1.7***, inauwezo wa kuhifadhi hadi kiwango cha ***GB 40***. Uwezo wa kipimo cha ***processor*** ni 1.7Ghz, kumbukumbu yake au ***memory ni 512***, na hifadhi yake au ***Hardspace*** ni ***GB 40…***

**2. John**: Hebu kodogo kwanza, niweze kuelewa vizuri zaidi kuhusu maneno haya ya kiteknolojia.

**SFX: Beep sound (should always be used to introduce the expert, like somebody answering in a quiz show)**

**3.Mtaalam**: Kipimo hiki cha ***Processor*** ni kasi inayowezesha komputa yako kufunguka au kushughulikia kile unachotaka kufanya katika komputa hiyo. Kasi hiyo hutegemea zaidi ukubwa wa kipimo hiki cha ***Processor***. Kipimo kikiwa kidogo,komputa yako itafungua polepole, na kikiwa kikubwa ndio kasi inavyongezeka. Kumbukumbu yaani ***Memory*** au kwa jina lingine la kiteknolojia ***RAM*** pia huathiri kasi ya Komputa yako . Hifadhi au ***Hard Sapce*** ambayo Timothy, meneja wa duka alikuwa akizungumzia pia inajulikana kama kisahani cha hifadhi yaani ***Hard Disk***. Hifadhi ya faili zako katika komputa hutegemea ukubwa wa kisahani hiki

**4. John**: Sawa, kwa hivyo Bw Timothy iwapo unataka kununua Komputa iliyotumika au kuu kuku, unapasa kuangalia nini hasa ?

**Clip: 2.1_Timothy_3**

Inategemea na uwezo o au bajeti yako. Kipimo cha chini kabisa unachopasa kuzingatia unaponunua Komputa kuu kuu, ni kwamba lazima iwe na uwezo wa Kumbukumbu yaani ***RAM 128*** ya kati ya ***20-40 GB,*** na pia vipimo hivi vinaweza kupanuliwa au kuongezwa bila malipo,..iwe na Skrini ambayo haijaharibika au kuvunjika na ni lazima komputa hiyo angalau iwe na huduma za kucheza ***DVD*** yaani ***DVD ROM,*** na iwe na uwezo wa kuchapisha na kunasa kanda za ***CD*** na ***DVD*** yaani ***CD,DVD Writer!***

**5. John:** Sawa, na je kuhusu Data au Programmu za Komputa yaani ***Software?***. Huwa zinakuja na data hizi au ni lazima niziweke mimi mwenyewe.?

**Clip: 2.1_Timothy_4**

Komputa tayari huwa na Data hizi . Kama unavyoona hii ni chapa halisi ya aina hii ya Komputa iitwayo ***Windows***, huwa na Data zake zilizowekwa na pia kinga dhidi ya virusi vinavyoweza kuharibu faili au Komputa yako yaani ***Anti Virus***, .

**6. John**: Hebukidogo . Iwapo Komputa hizi zimewekwa Data hizi, sasa nini unachopasa kuzingatia zaidi?

**Clip: 2.1Timothy_5**

Ni vyema kwanza kujua iwapo Data hizi ziko kwenye komputa yako, iwapo zimeidhinishwa au zina leseni, la sivyo itakuwa vigumu kuweka Data zako nyingine baadaye. Pia ni vyema kuchunguza iwapo Data hizi ziliwekwa vizuri.

**SFX_Karakana na vifaa**

**SFX: Beep sound (should always be used to introduce the expert, like somebody answering in a quiz show)**

**7. Mtaalam**: Anachomaanisha Timothy, ni kwamba unapasa kuchunguza na kuhakikisha kila kitu kiko sawa!. Unaweza kuona kwamba Data hizi zimewekwa lakini unapoanza kutumia komputa yako unakuta hazijawekwa au zimewekwa makosa.

**8. John**: Sawa. Timothy pia umezungumzia kinga dhidi ya Virusi katika Komputa yaani ***Anti Virus***. Kinga hii inamaana gani kwa komputa?

**Clip: 2.1_Timothy_6**

Kinga hii ni lazima uwe nayo kwenye Komputa yako la sivyo huenda ikaharibu au hata kukwamisha kabisa Komputa. Na mara nyingi waliokuuzia wanaweza kukataa kukurekebishia unapowarudishia wakisema tayari ilikuwa na Virusi ambavyo vimeathiri Data au Programmu zako. Kwa hivyo ni lazima uhakikisha imewekwa kabla ya kununua Komputa yoyote

**X-fade SFX_Karakana ikiwa na vifaa**

**SFX_Mlango wa Karakana wafunguliwa**

**9. John**: Na je Timothy, kuna vidokezo zaidi kwa Mtu kama mimi anayetaka kununua Komputa kuu kuu au ***Laptop***?

**Clip: 2.1_Timothy_ 8**

Ni lazima ununue Komputa kwa muuzaji anayeaminika, ambaye unaweza kumrudishia Komputa hiyo wakati inapokuwa na matatizo, sio kutoka kwa muzaaji wa vichochoroni au wapiti njia. Ni ni lazima upata dhamana ya Komputa yako unapoinunua, risiti ikiwa na anuani zote za muuzaji huyo.

**Muziki – Full up for 0:10 then fade under**

**SFX_ Komputa yafunguliwa SFX_Beep**

**1 Komputa**: Karibuni tena John na Beatrice. Nafurahi kuwa nanyi tena.

**2. John:** Tunahitaji usaidizi wako!

**3. Komputa**: Sawa kabisa, hapa mutapata majibu ya maswali yenu.

**4.Beatrice:** Tunataka kununua Komputa kuu kuu aina ya ***Laptop***. Lakini hatujui ni Data gani tunapasa kuhakikisha kabla ya kununua Komputa hiyo.

**5. John:** Sasa tutaanzia wapi.?

**SFX_ Komputa ikifunguliwa**

**6. Komputa**: Tuanzie mwanzo kabisa. Kwanza ni lazima muhakikishe kuwa Komputa hiyo ina mfumo halisi wa kufanya kazi. Yaani ***System.***

**7. Beatrice:** Ohhh…Tayari nimetatizika.

**8 Komputa**: Usitatizike Beatrice. Mfumo huu ndio unaoiwezesha Komputa yako kufungua Faili, kuhifadhi na kupanga Programmu katika Komputa yako. Kuna mifumo mitatu unayopasa kuzingatia…..

**9.Beatrice**: Mifumo hiyo inaitwaje?

**10. Komputa**: Kwanza kabisa kuna huu mfumo unaojulikana kama ***Windows***. Huu ndio mfumo unaojulikana zaidi ambao nautumia kwa sasa. Unakumbuka sauti hii?…

**SFX_Ukurasa wa Mfumo wa Windows ukifunguka.**

**11. John:** Ndio…

**12. Komputa:** Hiyo ndio sauti ya Mfumo huu unapoanza kufunguka. Asilimia 90 ya Komputa hutumia sana mfumo huu wa ***Windows.***

**13. Beatrice:** Kwanini?

**14Komputa** : Kwa kuwa mfumo huu wa ***Windows*** umetokea kuwa maarufu sana, Data au programu yaani ***Software na Hardware*** zinazotumika katika mfumo huu hupatikana kwa urahisi.

**15. Beatrice**: Kwa hivyo huu ndio mfumo tunaohitaji?

**16. Komputa**: Pengine, lakini msisahau nimetaja mifumo mitatu. Mfumo mwengine ni ule wa aina ya ***Mac.***

**SFX Mfumo wa MacOS ukifunguka**

**18. Komputa** : ***Mac*** ni ufupisho wa ***Macintosh***. Pia unaweza kupata Data za Mfumo huu lakini si rahisi ikilinganisha na zinazotumika katika mfumo wa ***Windows.***

**19. Beatrice:** Na wa tatu?

**20.Komputa**: Wa tatu unajulikana kama ***Linux.*** Huu umekuwa ukitumika kwa zaidi ya miongo mitatu. Mfumo huu sasa unatumika sana kuunganisha zaidi ya asilimia 90 ya mitandao. Ni mfumo unaoaminika lakini unatatiza kuuweka na hata matumizi yake.

**23. Beatrice**: Kwa hiyo si mzuri kwa watu wanaoanza kujifunza komputa kama John na Mimi ?

**24. Komputa**: Kwa kweli haumfai nyinyi kwa sasa.

**25. John**: Sasa tukijua ni mfumo gani tuanotaka, ni yapi mengine tunayopasa kuzingatia?

**26. Komputa**: Sasa itategemea Matumizi yako, unataka kufanya nini na ***Laptop***…

**27. Beatrice**: Nataka kutumia kwa kazi zangu za shule na kuandika barua..

**SFX Akipiga chapa**

**28. Komputa**: Unahitaji kuhakikisha kuwa komputa yako ina huduma za kupiga chapa au kuandikia barua zinazofahamika kama ***Microsoft Word***

**29. Beatrice**: ***Microsoft*** ni nini?

**30. Komputa**: Ni moja wapo ya kampuni zinazoaminika zaidi. ***Microsoft*** pia hutengeneza mfumo wa ***Windows.***

**33. John**: Sasa nimekuwa mwanasayansi chipukizi.. Na nikitaka kuchora grafu au kufanya hesabu ngumu?

**SFX computer mouse on table**

**34. Komputa.**: Utahitaji huduma maalum zinazofahamika kama ***Microsoft.*** Iwapo wewe ni mtu wa kutumia sana huduma hizi, basi unahitaji kununua programu itwayo , ***Microsoft Office***.

**35. Beatrice**: Hii ina nini?

**36. Komputa**: Programmu hii ina huduma kama vile ***Word, Excel na Power Point*** . Pia unaweza kupata programu hizi kwa ***Macintosh***

**37. John**: Na je iwapo natakua kutumia komputa yangu kwa …..

**8. Beatrice**: Tumefaulu …

**SFX_Muziki**

**39. John**: … Inacheza Muziki !

**40. Komputa**: Kwani nini isicheze! Ukitaka hudumaza kucheza muziki kwenye Komputa yako, basi unahitaji Programmu maalum ya kucheza muziki inayofahamika kama ***Media Player*** . Ikiwa unatumia mfumo wa ***Microsoft Windows***, basi unahitaji programu za ***Windows.*** Yaani ***Window's Media Player***, au ***Real Player***. Programu hizi ni kama maktaba ya Muziki kwenye Komputa yako.

**43. John:** Nini ? Vitabu?

**44. Sauti ya Komputa**: Hapana John. Utafurahia programu hizihizi.

**SFX_Filamu (Chagua filamu kwa mfano ya James Bond)**

**45. John**: Inacheza ***DVD .*** Ajabu !!

**46. Beatrice**: Nina Kamera…

**SFX_Camera_Click.** Sasa nahitaji nini kuhamisha picha zangu kutoka kwa kamera hadi kwa Komputa?

**47. Komputa** : Ukitumia au kuchagua huduma inayofaa ya ***Media Player*** pia utaweza kutazama picha zako kwenye Komputa.!

**48. John**: Ni hayo tu tunayohitaji?

**49 Komputa**: Hizi ni baadhi tu ya programu au huduma za kimsingi. Kwa kutumia huduma na mifumo yote niliyozungumzia hapo awali, utaweza kutumia komputa yako bila matatizo.

**52. John/Beatrice**: Asante sana Komputa.

**53. Computer**: Kila la kheri!

**SFX_ Mfumo wa Windosws ukifungwa kwenye Komputa.**

**SFX_Komputa ikifungwa..**

**Outro:**

Na ni hayo tu tuliyoweza kuwaandalia katika kipindi cha leo katika mfululizo wa vipindi kuhusu huduma za Komputa na Intaneti. Na usisahau kuulizia kuhusu dhamana unaponunua Komputa kuu kuu. Kumbuka ukitaka kukisikiliza tena kipindi hiki tembelea mtandao wetu wa www.dw-world.de/lbe. Hadi wakati mwengine kwaheri kwa sasa.